



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KAHAWA TANZANIA

TANGAZO

UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2021/2022

Utangulizi

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anawatangazia ufunguzi wa msimu mpya wa ununuzi wa kahawa kwa mwaka 2021/2022. Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa kanuni ya 23 (1) ya Kanuni za Kahawa 2013. Tarehe za ufunguzi wa msimu wa kuanza kwa ununuzi wa kahawa katika kanda za uzalishaji kahawa ni kama ifuatavyo;

Na.	Kanda	Mkoa	Tarehe ya Ufunguzi
1.	Kaskazini	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 Julai, 2021
2.	Mbeya, Songwe	Mbeya, Songwe, Katavi	15 Juni, 2021
3.	Kigoma	Kigoma	1 Mei, 2021
4.	Mara	Mara, Mwanza	1 Mei, 2021
5.	Kagera	Kagera	1 Juni, 2021
6.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 Julai, 2021

Mambo muhimu ya kuzingatia katika msimu huu 2021/2022:

- Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa wawape wanunuzi binafsi wa kahawa watakaomba vibali vya kununua kahawa kwenye Halmashauri zao kabla ya tarehe ya kuanza msimu ikiwa ni moja ya masharti yaliyotolewa ili kupata leseni ya ununuzi wa kahawa kwa mujibu wa Jedwali la Tatu la Kanuni za Kahawa 2013 na endapo Halmashauri itachelewesha au kukataa kutoa kibali pasipo sababu za msingi, Bodi itatoa leseni kwa mujibu wa kanuni ya 26 (2) ya Kanuni za Kahawa, 2013.
- Katika msimu huu mpya Bodi ya Kahawa Tanzania itaendelea na utaratibu wa kuendesha minada katika kanda za uzalishaji kahawa katika maeneo ya yafuatayo:
 - Bukoba:** Kwa ajili ya Mikoa ya Kagera, Mwanza – Minada itaendeshwa kama kutapatikana kiasi cha kahawa cha kutosha kuendesha minada.
 - Mbozi:** Kwa ajili ya Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa na Katavi

- **Mbinga:** Kwa ajili ya Mikoā ya Ruvuma na Njombe
- **Moshi:** Kwa ajili ya mikoa ya Kanda ya kaskazini

Minada ya kanda itaendelea kuwa ni ya kahawa safi na itafanyika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za uendeshaji minada zilizopo. Wakulima wanaruhusiwa kuuza kahawa yao kwenye mnada wowote ili kuwahi mzunguko wa minada.

3. Maombi ya leseni zote mpya na maombi ya kuhuisha (renew) leseni yatafanyika kwa njia ya mtandao katika mfumo wa ATMIS kwa kufuata kiungo cha <https://atmis.kilimo.go.tz>.
4. Vyama vya ushirika vinatakiwa kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima mara tu inapokuwa tayari na kuipeleka kahawa hiyo kwenye viwanda vya kukoboa kahawa. Aidha, vyama vya ushirika vitapaswa kuhakikisha kuwa akaunti zao za malipo zipo hai ili kuwezesha zoezi la uuzaji wa kahawa na malipo kufanyika mapema na kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya fedha za wakulima.
5. Vyama vya msingi vitakavyouza kahawa mnadani vitaomba vibali vipya kwa kutoa taarifa ya kuomba upya vibali kwa kujaza fomu ya kuhuisha vibali. Fomu hizi zinazopatikana kwenye ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa na viwanda vya kukobolea kahawa na watasaidiwa kuomba vibali katika mfumo wa ATMIS na maofisa waliopo kwenye ofisi za kanda za Bodi ya Kahawa.
6. Vyama vya ushirika vikamilishe mapema taratibu za upatikanaji wa mitaji ili vianze ukusanyaji wa kahawa ya wakulima wao mara tu kahawa inapokuwa tayari.
7. Bodi ya Kahawa itaanza mara moja kuendesha minada ya kahawa pindi kiasi cha kutosha cha kahawa kitakapokuwa tayari.
8. Bodi itatoa mwongozo wa masoko ya kahawa kwa msimu huu ili kutoa ufafanuzi na maelekezo mapema iwezekanavyo.
9. Vyama vya ushirika vihakikishe kuwa mitambo ya kuchakata kahawa (CPU) iliyoko katika maeneo yao inatumika na inafunguliwa mara tu kahawa inapokuwa tayari ili kufanikisha lengo la Serikali la kuongeza ubora wa kahawa na bei ya mkulima.



Mkurugenzi Mkuu

Bodi ya Kahawa Tanzania

S. L. P. 732 – Moshi, Simu: 027-27-52324; Nukushi: 027-27-52026

Barua pepe: info@coffeeboard.go.tz; Tovuti: www.coffeeboard.or.tz